*Mulika, Juz. 44(2), 291-312*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Urudiaji wa Kisufi na Motifu kama Mtindo Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*

*Aloo Ronald Odhiambo*[1] *na Kineene wa Mutiso*[2]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.8

**Ikisiri**

Makala hii inashughulikia aina na mchango wa urudiaji wa kisufi na motifu katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Urudiaji wa kisufi na motifu mbalimbali vimejitokeza kwa viwango mbalimbali katika utungo huu. Vipengele hivyo ndivyo misingi ya fani na maudhui katika utenzi huu. Licha ya kazi na umuhimu wa vipengele hivyo kuchunguzwa sana katika tenzi za Kiswahili, kwa uelewa wetu, hakuna uhakiki wa kina uliofanywa kuvihusu kama mitindo katika utenzi. Hivyo, lengo la makala hii ni kuhakiki kwa kina urudiaji wa kisufi na motifu kama mitindo iliyofanikisha fani na maudhui katika utenzi. Tumegundua kuwa matumizi ya mtindo wa urudiaji wa kisufi, motifu na vipengele vyake ndiyo msingi na kiini cha fani, maudhui, na maana katika utenzi. Nadharia ya Umitindo ya Geoffrey Leech (1969) ndiyo iliyotumika kwani inasaidia kuhakiki na kutoa fasiri kwa kazi za isimu na fasihi kwa sababu uchunguzi wa vipengele vya kifasihi hauwezi kujisimamia. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani na ulitumia mbinu ya usomaji matini. Utenzi tajwa uliteuliwa kimakusudi na data zimewasilishwa kimaelezo. Imebainika kuwa mtunzi ameonesha matumizi ya usufi kupitia motifu ya safari, ndege, na mwanga. Urudiaji huu wa kisufi unachangia uendelezaji wa dhamira ya kidini, toba, siku ya kiyama, wahusika, maudhui, na kuleta mwangwi wa kidhamira na usisitizaji.

## 1.0 Utangulizi

Katika kazi hii, tumeshughulikia aina na mchango wa urudiaji wa kisufi na motifu katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Aloo na Wa Mutiso (2023) wanaeleza kuwa urudiaji ni mbinu ya kifasihi ambayo inahusu kutumiwa tena na tena maneno yaleyale au vifungu vya maneno mara chache ili wazo liweze kuwa wazi na tena likumbukwe zaidi. Mtunzi anapotumia takriri katika utenzi, basi anafanikisha fani na maudhui katika kazi hiyo. Sababu ni kwamba urudiaji ni mojawapo ya mitindo ambayo inatumiwa na mtunzi kuleta mshikamano katika utungo (Wamitila, 1999). Tannen (1989) anasema kuwa urudiaji wa neno au kifungu cha maneno hutumiwa na mtunzi kuongeza msisitizo, kuboresha au kuimarisha ushawishi kuhusu jambo katika utenzi. Isitoshe, matumizi ya urudiaji huongeza nguvu kwa yale yanayozungumziwa. Croft na Robert (2000) wanaeleza

[1] Mhadhiri, Idara ya Elimu na Masomo ya Mbali, Ndaki ya Elimu na Mafunzo ya Nje, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Baruapepe: alooronald@gmail.com
[2] Profesa, Mhadhiri Mkuu, Idara ya Kiswahili, Kitivo cha Sanaa, Chuo Kikuu cha Nairobi, Kenya. Baruapepe: kineenewamutiso@yahoo.com/ mkineene@uonbi.ac.ke

kuwa matumizi ya urudiaji katika kazi humsaidia mtunzi kukuza wazo lake katika kazi ambayo ndiyo mahitaji ya msingi ya mitindo.

Wa Mutiso (2005) anafafanua kuwa usufi ni kujitolea mhanga kwa hali na mali ili kumtumikia Mwenyezi Mungu kwa kutafuta maarifa ya moyoni kuhusu Mungu na imani. Tunaweza kusema kuwa kanuni zinazoongoza usufi ni kama vile uaminifu, toba, ukumbusho na upendo. Aidha, Wa Mutiso anasisitiza kauli hii kwa kusema kuwa ni kutomiliki ama kutomilikiwa na zaidi, ni kutochoka kudadisi au kusaili wala kuvunjika moyo, kwa sababu ya vionjo vya dunia.

Naye Schaeder (1935) anaeleza kuwa usufi wa Kiislamu ni jaribio la kuufikia wokovu wa mtu binafsi kwa kupata tauhidi. Tauhidi ni kuutambua na kuudumisha umoja au upweke wa Allah katika maneno, vitendo na itikadi ama imani zetu zote. Ni istilahi inayomaanisha kumpwekesha Mwenyezi Mungu katika ibada, kumwabudu yeye peke yake bila ya kumshirikisha na kitu chochote. Tauhidi ni kutangaza kwamba Mungu ni mmoja tu na hapana mfano wake. Tauhidi ni muhimu katika usufi kwa sababu inamsaidia msufi kusamehewa dhambi zake, kuepushwa na kukaa motoni milele. Badala yake msufi huwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu na pia hupata amani kamili na wongofu hapa duniani na kesho akhera.

Hivyo basi, kwake Wa Mutiso (2005), masufi humhusudu Mungu kuliko mtu au kiumbe kingine, naye Mungu, kwa maoni yao, huwahusudu kuliko kiumbe kingine. Vilevile, masufi wanasema kuwa usufi unaongozwa na kanuni za Umungu, isitoshe, wanaeleza kuwa ni njia ya usufi (*tariqa*) na mwisho ni ukweli. Hivyo basi, kuna masufi wa shia wanaojinasibisha na Kuruani na mafundisho ya Mtume Muhammad tofauti na masufi wasio wa shia ambao wana utawala maalumu wa kiroho na wa kisiasa juu ya umma. Masufi wa shia huamini katika imani za kifalsafa na mienendo ya kiroho. Geoffrey (2010) anasema kuwa usufi unaweza kufafanuliwa kama kipengele cha hekima ya milele. Mtunzi wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* ametumia urudiaji wa kisufi na motifu ili kuleta athari mahususi katika utenzi huu. Katika mkabala huu, tumechunguza urudiaji wa kisufi na motifu kama mitindo ambayo inafanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

## 2.0 Muhtasari wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*

*Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* ulihaririwa na Knappert mnamo 1964, hata hivyo, mtunzi wake hajulikani. Utenzi huu una beti mia saba sabini na sita (776). Katika beti hizi, mtunzi amezungumzia masuala mbalimbali kama vile suala la uumbaji ambapo mtunzi anaelezea kuwa Mungu aliumba vitu vingi ila vinne pekee ndivyo vitakatifu. Vitu hivi ni pamoja na malaika wanne, milima minne, siku nne na wanawake wanne. Knappert (1964) anaeleza kuwa utenzi huu umegawanywa katika sehemu nne. Katika sehemu ya kwanza, mtunzi ametaja kisa

cha Ali bin Talibi akiyajibu maswali ya mgeni Mudhari bin Darimi anayewasili Meka pindi tu baada ya kifo cha Mtume Muhammad. Sehemu ya pili (ubeti 553-591) ina hadithi ya Ibilisi akimhoji Mtume Muhammad na akimwelezea kuhusu watu anaowapenda. Sehemu ya tatu (ubeti 592-665) inaelezea kuhusu majukumu mbalimbali katika Uislamu na sehemu ya nne (ubeti 666-704) inahusu mahubiri ya Abu Bakari kuhusu majukumu haya. Aidha, katika utenzi huu, mtunzi anazungumzia maswali ishirini yanayoulizwa na Mudhari bin Darimi kwa Sheikh Ali. Sheikh Ali kama mtetezi wa dini ya Kiislamu, anapata ufunuo na kuyajibu maswali hayo. Maswali haya, ndiyo misingi ya hukumu siku ya kiyama. Aidha, Mwislamu anashauriwa na mtunzi kuyazingatia mambo haya kwa sababu ndiyo kiini cha Uislamu. Maswali haya yanaangazia mambo mbalimbali kuhusu dini. Katika utafiti huu, tumejikita katika kuchunguza namna mtunzi anavyotumia urudiaji wa kisufi na motifu katika kuwasilisha fani na maudhui katika utungo huu.

## 3.0 Msingi wa Nadharia ya Umitindo

Mtindo hurejelea namna ambavyo mtunzi anatumia lugha yake kulingana na muktadha ili kuwasilisha ujumbe. Kwa mujibu wa Abrams (2015), Nadharia ya Umitindo inachunguza sifa kama vile urudiaji katika kazi. Wamitila (2008) anaeleza kuwa nadharia hii ilitokana na Nadharia ya Balagha iliyokuzwa na kuendelezwa katika jadi ya Kiyunani na Kirumi na wataalamu kama vile Aristotle, Plato na Cicero katika karne ya 15 (384-322). Nadharia ya Balagha ilithamini jinsi ya kuzungumza au kuwasilisha ujumbe kwa njia ya maandishi. Wamitila (2008) anasisitiza kuwa kimsingi, Balagha ilidhamiriwa kufundisha njia zifaazo za kuushawishi umma. Msisitizo wake mkubwa ulikuwa kwenye mazungumzo yafaayo na ulumbi wa kushawishi. Kwa sasa Nadharia ya Umitindo inajisimamia na hata kutumiwa katika uhakiki mbalimbali katika ushairi. Geoffrey Leech ni mtaalamu wa kwanza aliyetumia mawazo ya Nadharia ya Umitindo katika ushairi. Leech (1969) anakariri kuwa nadharia hii inatumiwa kuhakiki na kutoa ufafanuzi kwa kazi za kifasihi na pia zile za isimu kwa sababu vipengele hivi vya kifasihi na kiisimu haviwezi kujisimamia. Aidha, ni vigumu sana kufafanua na kuainisha vipengele vya kifasihi kama vile urudiaji na usufi bila kurejelea vipengele mbalimbali vya kiisimu.

Aidha, Leech (1969) anabainisha yafuatayo kuhusu lugha na fasihi. Kwamba, kwa kiwango kikubwa mtindo ndio huleta athari kwa matini. Mtindo unahusu namna ambavyo lugha hutumiwa na, haujabanwa katika fasihi pekee, bali ni sehemu ya usemi wowote, kwa vile msemaji ana uhuru wa kuchagua namna ya kuzungumza katika muktadha wake. Leech anaendeleza mjadala huu kwa kusisitiza kuwa Nadharia ya Umitindo inasaidia katika kubainisha sheria ambazo zinatumiwa kuteua maneno maalumu katika lugha ambayo inatumiwa kutekeleza shughuli tofautitofauti za jamii zinazouhusisha utoaji na upokezi wa maana ya ujumbe na hata uchanganuzi wa diskosi na fasihi. Hivyo basi, katika utenzi, mtunzi ana idhini ya kutumia urudiaji wa kisufi ili kupitisha ujumbe wake kwenye utungo.

Aidha, Crystal na Davy (1969) wanachangia katika Nadharia ya Umitindo kwa kusema kuwa nadharia hii inachunguza lugha ili kubainisha sifa zake mahususi zinazopatikana katika muktadha maalumu kutoka katika sifa za kiisimu ambazo ni za kijumla. Sifa hizi huwa zinapatikana katika muktadha wa matumizi ya lugha. Mawazo haya yanatusaidia katika kuchunguza namna urudiaji wa kisufi na motifu ulivyotumiwa kama mtindo katika kazi yetu.

Nadharia ya Umitindo inasaidia katika kuchunguza kisemwacho na namna kinavyosemwa. Wazo hili limetusaidia katika kuchunguza namna mtunzi anavyotumia urudiaji wa kisufi na motifu kama njia ya kufanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Wamitila (2003) anaendeleza mjadala huu kwa kusema kuwa Umitindo ni nadharia inayotumiwa kuchunguza vile matukio tofautitofauti yanavyoelezwa katika isimu na fasihi kwa kutumia lugha.

Wataalamu kama vile Leech (1969), Simpson (2004) na Wamitila (2008) wameorodhesha vipengele vinane muhimu vinavyostahili kuchunguzwa katika uhakiki wa kimitindo. Vipengele hivi vimejumuisha uteuzi na mitindo, lugha ya kitamathali na mitindo, usimulizi na mitindo, sarufi na mitindo, uchimuzi na mitindo, mitazamo na mitindo, itikadi, mishikamano na mitindo, muwala, uzungumzaji na mbinu zinazotumiwa kuwasilisha usemi na mawazo.

Wamitila (2008) anapiga hatua kwa kuvitolea ufafanuzi vipengele hivi. Hata hivyo, hatujashughulikia vipengele hivi vyote katika makala hii. Tumeshughulikia tu kipengele cha uchimuzi na mtindo kwa vile ni faafu zaidi katika kuchunguza urudiaji wa kisufi na motifu kama mbinu ya kimitindo inayofanikisha fani na maudhui katika utenzi wetu. Wamitila (2008) anasisitiza kuwa mtafiti anapotumia uhakiki wa kimitindo, ni lazima ateue baadhi ya vipengele vya kuchunguza kwa vile ni vigumu kuvichunguza vipengele vyote kwa undani.

Katika utafiti huu tumeongozwa na kipengele cha uchimuzi na mtindo. Kipengele hiki kinashughulikia namna ambavyo mtunzi amekiusha lugha yake kwa kutumia urudiaji wa kisufi ili kuweka wazi ujumbe wake katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* kama njia ya kufanikisha fani na maudhui kwenye utungo huu (Aloo na Wa Mutiso, 2023). Chapman (1974) kwa upande wake, anaeleza kuwa urudiaji wa kisufi ni uchimuzi wa kimtindo unaotokana na ukiushi wa lugha na ambao unatumiwa na mtunzi akiwa na lengo la kuweka wazi jambo analolizungumzia.

Mihimili ya Umitindo inayotuongoza katika utafiti wa makala hii ni: mosi, ujumbe katika kazi ya kifasihi hutokea katika mtindo wa urudiaji wa kisufi unaohusika. Pili, vipengele vya lugha kama vile mbinu ya urudiaji wa kisufi na ujumbe, vina uhusiano mkubwa na haviwezi vikatenganishwa. Mihimili hii miwili imetusaidia

katika kutambua namna ambavyo urudi aji wa kisufi umetumiwa na mtunzi. Vilevile, tumeweza kubainisha namna ambavyo urudiaji huu wa kisufi unahusiana na ujumbe na kujenga fani na maudhui. Nadharia hii imetusaidia katika kuchunguza kinachosemwa na mtunzi na namna kinavyosemwa kupitia mbinu ya urudiaji, usufi na motifu. Vilevile, nadharia hii imetusaidia katika kufahamu namna mtunzi anavyokiusha lugha yake kupitia mtindo wa urudiaji, usufi na motifu ili kuwasilisha ujumbe wake.

**4.0 Uchanganuzi**

Mtunzi wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* ametumia urudiaji wa kisufi katika kuangazia masuala tofauti kwenye utungo wake. Urudiaji wa kisufi na motifu mbalimbali zimetokea katika viwango mbalimbali katika utenzi husika. Isitoshe, vipengele hivyo ndivyo misingi ya fani na maudhui katika utenzi huu. Licha ya kazi na umuhimu wa urudiaji wa kisufi na motifu katika tenzi za Kiswahili, kwa uelewa wetu, hakuna uhakiki uliofanywa katika vipengele hivi, licha ya utenzi kuchunguzwa sana. Yaliyomo yanahusu mambo ya kijumla kuhusu urudiaji wa kisufi na motifu ambayo hayajashughulikia umuhimu na majukumu haya. Kazi nyingi hazijahakiki kwa kina urudiaji wa kisufi na motifu kama mitindo katika utenzi. Tumebainisha jinsi mtunzi huyu alivyotumia urudiaji wa kisufi (motifu na ishara) kama mbinu ya kufanikisha fani na maudhui. Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Tumesoma majarida na vitabu vilivyoandikwa kuhusu utenzi, urudiaji wa kisufi, motifu na Nadharia ya Umitindo ambayo imetuongoza katika utafiti wetu. Tumedondoa beti zinazofaa ili kuthibitisha madai yetu kulingana na suala tunalolijadili. Tulichagua utenzi huu kusudi. Tumetumia maelezo na ufafanuzi kuwasilisha data yetu. Baada ya uhakiki wetu, tumegundua kuwa mtunzi ameonesha matumizi ya usufi kupitia motifu ya safari, ndege na mwanga. Isitoshe, mbinu hii ya urudiaji wa kisufi ndiyo msingi wa kuelewa ujumbe wa utenzi huu kuhusu toba, siku ya kiyama na masuala ya uumbaji. Vipengele tulivyovishughulikia katika makala hii ni: dhana ya urudiaji, fasili ya usufi na motifu katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, motifu ya safari ya ndani na nje, motifu ya ndege na motifu ya mwanga. Ili kufikia lengo letu, tumeongozwa na mihimili miwili ya Nadharia ya Umitindo.

**5.0 Urudiaji katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi***

Aloo na Wa Mutiso (2023) wanaeleza kuwa urudiaji ni mbinu ya kifasihi inayohusu urejelezi wa matumizi ya sauti, neno, kirai au kishazi, mishororo na beti kwa kusudi la kuleta athari kuhusu kile kinachozungumziwa au kilichoandikwa. Urudiaji wa maneno yaleyale au virai katika kazi ya kifasihi kama vile utenzi, ushairi au kazi ya kinathari unaweza kuleta uwazi wa wazo na pia unaweza kumsaidia msomaji kukumbuka wazo hilo. Mbali na urudiaji kusaidia katika kusisitiza au kuonesha mawazo au hoja muhimu, urudiaji unaweza kuwa chombo muhimu kwa watunzi na wasemaji katika kuendeleza mtindo na wizani. Kwa mfano, katika utenzi huu, mtunzi amerudia sauti na silabi katika beti mbalimbali ili

kufanya ujumbe wake kukumbukika. Vilevile, sauti na silabi hizi zimetumiwa mwanzoni na mwishoni mwa mishororo mbalimbali ili kuleta mdundo katika utenzi. Hilo linathibitika katika ubeti huu:

> ***Wa**li zijana wawi**li**,*
> ***Wa**po mahala pamba**li**,*
> ***Wa** katika filiha**li**,*
> *Zikawa zita thakiya*. (ubeti wa 238)

Katika mifano hii, silabi **wa** na **li** zimerudiwa mwanzoni na mwishoni mwa mishororo hii mitatu. Urudiaji huu wa sauti **w**, **a**, **l** na **i** unachangia katika kuleta mahadhi na mdundo katika ubeti huu na kufanya ujumbe wa ubeti kukumbukika. Kupitia mtindo huu wa urudiaji, mtunzi ameeleza hali ya Habila baada ya kuuliwa na nduguye Kabila. Tukio hili linatokea kwenye utenzi baada ya Habila kukataa kuolewa na nduguye.

## 6.0 Fasili ya Usufi katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*

Tunapojadili usufi, Nadharia ya Umitindo imetusaidia katika kufanya hivyo. Sababu yake ni kuwa, nadharia hii inachunguza kisemwacho na namna kinavyosemwa. Wazo hili limetusaidia katika kuchunguza namna mtunzi anavyotumia urudiaji wa kisufi kama mtindo wa kufanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Utafiti huu umeshughulikia usufi kama mtindo wa urudiaji unaotumiwa na mtunzi kuwasilisha dhamira mbalimbali. Aidha, mtindo huu wa usufi ndio msingi wa maana inayowasilishwa na mtunzi.

Schaeder (1935) anafafanua kuwa historia ya usufi inatokana na maoni ya masufi kuwa Mtume Muhammad ndiye sufi wa kwanza. Sababu yao ni kwamba masufi huamini kuwa nuru iliumbwa kwanza na Mungu kabla ya Adamu. Aidha, nuru hii ni ishara ya Mtume Muhammad. Hivyo, Mtume alikuwako hata kabla ya kuumbwa kwa Adamu. *Kuruani Tukufu* ndiyo ilhamu ya usufi. Kulingana na Waislamu, kupanda kwa Mtume Muhammad mbinguni na kuonana na Mungu ni kielelezo kwa kila sufi kujihisi kuwa yuko mbele ya Mungu.

Al-Bukhari (1989) anafafanua ya kwamba kupanda kwa Mtume Muhammad mbinguni kumesimuliwa katika kisa cha Israi na Miiraji hasa pale ambapo Mtume Muhammad anakutana ana kwa ana na Mungu anapofika mbingu ya saba huko Mkunazi wa Mwisho au Sidratil Muntaha. Katika kisa hiki Mtume Muhammad alipandishwa kwenye uwingu wa saba ambako alikutana na Ibrahimu, akamsalimia naye akamjibu salamu yake, akamkaribisha na akaukubali utume wake. Baada ya hapo, alinyanyuliwa hadi Mkunazi wa Mwisho na akapandishwa

kupelekwa kwa Allah (Mungu) mwingi wa utukufu. Akasogea Nabii mpaka umbali wa kiasi cha masafa ya pinde mbili au karibu zaidi kuliko hivyo.
Al-Bukhari (1989) anayaendeleza haya kwa kueleza kuwa katika kisa hiki, Mungu alimfunulia Mtume Muhammad kwa kumpa amri kuwa wasali mara hamsini. Mtume Muhammad alizipokea amri hizo na kisha akaanza kurejea mpaka alipofika mahali alipokuwa Nabii Musa. Alipofika kwa Musa, alimuuliza amri alizopewa. Mtume Muhammad alimwelezea kuwa alipewa amri ya kwamba wasali mara hamsini. Musa akamwambia kuwa hakika Umma wa Kiislamu hawataweza kutekeleza jambo hilo, kwa hivyo akamshauri kuwa arejee kwa Mwenyezi Mungu ili aombe kupunguziwa. Mtume Muhammad akageuza uso na kumwangalia Malaika Jibrili kwa jicho la kutaka ushauri katika jambo hilo, naye akampa ishara ya ndiyo kama ukitaka.

Kwa mujibu wa Al-Bukhari (1989), Mtume Muhammad alipanda na Jibrili mpaka akafika kwa Mungu. Mungu akampunguzia sala kumi kisha akateremshwa mpaka mahali alipokuwa Musa na akamwelezea kuhusu idadi ya sala zilizopunguzwa. Musa akamshauri kuwa arejee tena kwa Mwenyezi Mungu ili amwombe apunguziwe sala zaidi. Mtume Muhammad hakuacha kwenda na kurudi kwa Musa na Mungu mpaka sala zikabaki tano. Hapo mtume Muhammad akajibu kuwa anaona haya. Vilevile, Mtume Muhammad akaeleza ya kwamba ameridhika na anakubali sala alizopewa. Jambo hili la sala limesheheni katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* na kuendeleza usufi msimulizi anapotuelezea kuhusu miezi minne na siku nne takatifu za kusali.

Katika utenzi huu, mtunzi anaeleza kuwa Mungu aliumba mwezi wa Muharamu, Rajabu Muhhashamu, Shaabani na Ramadhani ambayo Mwislamu ametengewa kuomba na kufunga. Msimulizi anasimulia kuwa Mungu aliumba siku nne takatifu. Siku hizi ni pamoja na siku ya Juma, Idi mbili na Arafa. Aidha, mtunzi anaeleza kuwa Mungu aliwatengea Waislamu siku bora. Siku hizi ni Lailatu I'Haji, idi mbili na Laila Miiraji yanayostahili kuheshimiwa katika dini ya Kiislamu. Mifano ifuatayo ni ithibati ya madai yetu:

*Kavuwa Mola Jalali,*
*Siku inne zilo mbali,*
*Akazipa manazili,*
*Zikashinda zote piya. (ubeti wa 50)*

*Juma haina mithali,*
*Pamoya na Idi mbili,*
*Na Arafa imenali,*
*Nimeziye kuwambiya. (ubeti wa 51)*

*Na masiku iliyo bora,*
*Aliyotenga Jabari,*

*Taweleza kula mara,*
*Mtakapo kusikiya.* (ubeti wa 52)

*Ni Lailatu I'Haji,*
*Na Idi thani sihuji,*
*Na Laila Miiraji,*
*Zimekwisha kutimiya.* (ubeti wa 53)

Katika beti hizi, mtindo huu wa urudiaji wa kisufi umetumiwa na mtunzi ili kuendeleza dhamira ya toba, utakatifu na dini kwa ujumla. Haya yanasisitizwa kupitia kwa Waislamu kutengewa siku maalumu ya kuomba.

Wa Mutiso (2005) anaeleza kuwa masufi wanamchukulia Mtume Adamu kama sufi wa kwanza kwa vile alikaa siku arobaini akiwa katika hali ya utawa kabla Mungu hajampa roho na taa ya akili katika moyo wake na mwangaza wa hekima katika ulimi wake. Vilevile, wanaeleza kuwa baada ya Adamu kufanya dhambi, alitubu Bara Hindi kwa muda wa miaka mia tatu hadi akachaguliwa na Mungu na akawa sufi halisi au mtakatifu.

Kwa mujibu wa Wa Mutiso (2005), sifa kuu ya usufi ni kutia maana au fasiri za kisufi katika kila herufi ya abjadi. Kila herufi huwa inaficha siri zake ambazo kila sufi huzifahamu. Hivyo, Mwislamu huitukuza abjadi ya Kiarabu kwa sababu huziona kama herufi ambazo zilitumiwa na Mungu kumfunulia Mtume Muhammad Kuruani Tukufu. Kwake Mwislamu kujua herufi za Kiarabu ni chombo cha wahayi na majina matakatifu. Isitoshe, sifa za Mungu huweza kuelezwa tu kwa kutumia herufi hizi.

Wa Mutiso (2005) anasisitiza kuwa, kwa mujibu wa masufi, hekima zote hupatikana katika herufi 'alif'. Herufi hii ndiyo herufi ya kwanza katika abjadi ya Kiarabu na ni mfano wa Allah. Masufi waliunda lugha yao ya siri kwa kutumia dhana zao za usufi kutokana na abjadi ya Kiarabu kama njia ya kuwaficha watu wa kawaida fikra zao. Washairi wa Kiislamu walifananisha makazi yao au sehemu za miili na herufi. Vilevile, masufi pia walieleza kuwa herufi zote katika lugha mbalimbali humsifu Mwenyezi Mungu. Masufi huamini kuwa Mungu aliziumba herufi na kujiwekea siri za herufi hizi lakini pindi alipomwumba Adamu alimfunulia siri hii bila kumfunulia malaika yeyote. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* mtunzi anatanguliza shughuli zake kwa sala maalumu kwa Mwenyezi Mungu. Utangulizi huu umetolewa katika lugha ya Kiarabu. Mfano katika utenzi:

*Bismillahi Wahidu,*
*Rahamani Li Swamadu,*
*Rahimu Rabbu Shahidu,*
*Hana kifani Jaliya.* (ubeti wa 12)

Katika ubeti huu wa utangulizi, msanii anaonesha imani yake katika dini kwa kuanza masimulizi yake kwa kumshukuru Mola na kutaja baadhi ya sifa zake. Matumizi ya mtindo huu wa urudiaji wa kisufi yanasaidia katika kuendeleza dhamira ya dini katika utungo.

Ushairi mwingi wa kisufi pamoja na washairi wengi maarufu walitoka huko Fursi (Uajemi). Ushairi wa kisufi huwa mgumu kwa sababu washairi wa kisufi huchota lugha ya zamani iliyochakaa kabisa kama tunavyoona katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* wenye maneno ya Kiarabu. Masufi huhusudu maisha ya peponi na hujinyima raha na utajiri wa dunia hii kama inavyoelezwa katika utungo wetu. Kwa msufi, dunia ni michezo na inapita kama tunavyoona katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* na utungo kama vile *al-Inkishafi* na *Utenzi wa Qiyama*.

Katika ubeti wa 640-653 wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, msanii anasimulia kisa cha kwenda peponi siku ya kiyama. Anasisitiza kuwa watakaoenda peponi ni watu wakarimu pekee. Aidha, anahimiza Waislamu kuwa waliokaidi amri za Mola wataumia na kuangamia siku hii. Kwa hivyo, ni kheri kutenda mema kuliko kutenda maovu.

*Na pepo ndangu Latifu,*
*Maulana Ashrafu,*
*Utwambiziye Sharifu,*
*Umati yangu sikiya. (ubeti wa 640)*

*Na twaa ndenu yuwani,*
*Sute mbwakufa twaani,*
*Waja tungiye peponi,*
*Tutiipo tutangiya.* (ubeti wa 641)

Masufi wote huamini katika mambo yafuatayo: kwanza, wanaamini kuwa Mungu yuko katika kila kiumbe na kuwa kila kitu kiko katika yeye. Pili, vitu vyote ambavyo vinaonekana na visivyoonekana ni ruwaza ya Mungu, vinatokana naye na kamwe haviwezi vikatofautiana naye. Suala hili limeangaziwa kwa undani sana katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* na tungo nyinginezo kama vile *Utenzi wa Qiyama* na *Utenzi wa Ayubu*.

Kwa mfano, shughuli zote za utungo huu na tungo nyinginezo za kidini zinaanza kwa sala za kumsifu na kutoa shukrani kwa Mungu na vilevile zinakamilika kwa sala. Masuala mbalimbali yanayoendelezwa na Mtume Muhammad, Isa, malaika, Nabii Musa anapowaokoa wana wa Israili, Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi yote yanaanza kwa Mungu na kutamatika kwake.

Katika ubeti wa 33-65, mtunzi anazungumzia namna ambavyo Mungu aliumba vitu vingi ila vinne pekee ndivyo muhimu zaidi. Mtunzi anasimulia kuwa baada ya Mungu kuumba vitu vinne vitakatifu, aliumba vitu vingine vingi ili kujaza dunia. Shughuli hii ya uumbaji inaanza kwa Mungu katika ubeti wa 33 na baada ya uumbaji shughuli zote zinakamilika kwa Mungu katika ubeti wa 65. Mtunzi anaelezea katika ubeti wa 65 kuwa sifa za Mungu ni nyingi ajabu kiasi kwamba hawezi akakamilisha kuelezea sifa hata moja. Kwa mfano:

*Sasa tawapa khabari,*
*Alipoumba Jabari,*
*Ruhu zalipokithiri,*
*Aliteuwa Jaliya. (ubeti wa 33)*

***Swifa za Mola Latifu***,
***Ni nyingi mno tukufu***,
***Nawezapi kuziswifu***,
*Kutimiza swifa moya.* (ubeti wa 65)

Tatu, Wa Mutiso (2005) anaeleza kuwa usufi ni falsafa ya kweli ya Kiislamu na ingawa dini zote zina uyakinifu, dini ya Uislamu ndiyo dini sahihi. Nne, masufi wanaeleza kuwa yakini hakuna tofauti kati ya ubaya na uzuri kwa sababu Mungu ndiye husababisha vitendo vyote vya kila mwanadamu.

Vilevile, wanaamini kuwa majaliwa ya kila mwanadamu hutokana na Mungu na, kwa hivyo, mwanadamu hana uhuru wa kuchagua hatima yake katika maisha. Aidha, masufi wanaamini kuwa roho iliumbwa kabla ya mwili na ni mfungwa wa mwili. Hivyo, ni furaha na matumaini ya sufi kufa ili roho irudi katika hali ya uhuru ya hapo mwanzoni. Wanasisitiza kuwa pana haja ya kuzitakasa roho za Waislamu kama njia ya kuziunganisha na Mwenyezi Mungu. Wajibu wa kila sufi ni kuiongoza roho ambayo inazurura na imemkimbia Mwenyezi Mungu hatua kwa hatua ili iweze kumrudia.

Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, mtunzi anazungumzia suala la nafsi katika beti mbalimbali na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kuendeleza urudiaji wa kisufi kama mtindo. Kwa mfano, katika ubeti wa 690-698, mtunzi amewasimulia Waislamu kuhusu hukumu ambayo wataipitia siku ya mwisho. Shughuli hii itatokea baada ya Waislamu kufariki na roho zao kufufuliwa na Mungu kwa ajili ya hukumu. Mtu wa kwanza kufufuliwa kulingana na dini ya Kiislamu ni Mtume Muhammad ambaye atawatetea Waislamu. Suala hili linathibitisha usufi katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Isitoshe, suala la hukumu limetawala katika utungo huu.

*Utwambiziye Hashima,*

*Siku nyuma ya Kiyama,*
*Kutatoka bora nyama,*
*Jahanamuni sikiya. (ubeti wa 690)*

*Tawambiya mufahamu,*
*Kula alo Isilamu,*
*Ni Harishati isimu,*
*Nayazidi kukweleya.* (ubeti wa 691)

Zaidi ya hayo, wanaeleza kuwa ni wajibu wa kila sufi kutafakuri ili aweze kuungana na Mwenyezi Mungu. Aidha, ni wajibu wa sufi kuzikumbuka sifa za Mungu kimoyomoyo pamoja na kupiga hatua katika kujiendeleza katika safari ya maisha ili aweze kuufikia umoja na Mwenyezi Mungu. Mwisho, masufi huamini kuwa maisha ya mwanadamu ni safari na muumini ni msafiri. Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* sawa na tungo nyinginezo za Kiislamu, mtunzi amezungumzia suala la safari kwa Waislamu kutoka uhai hadi kifo. Aidha, Waislamu wanafunzwa njia mbalimbali wanazoweza kutumia ili wamkaribie Mungu.

Msisitizo wa usufi katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* na tungo nyinginezo za Kiislamu ni juu ya uhusiano wa moja kwa moja na Mungu anaoupata Mwislamu kutokana na mazoea yake ya kumkumbuka Mungu. Ushairi wa kisufi kama vile *Utenzi wa Qiyama*, *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, *Utenzi wa Ngamia na Paa* na *Utenzi wa Ayubu* huonesha mafundisho ya *Kuruani* yenye maana ya kindani. Dhana hazifasiriwi kwa njia ya moja kwa moja bali maana yake ni ya kitamathali. Kwa mfano, kulewa haimaanishi ‘kunywa pombe’, ina maana ya ‘kulewa kwa maneno ya Mungu au katika dini’. Mfano katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*:

*Mambo mane Isilamu,*
*Awapo nayo ni tamu,*
*Tena imetulazimu,*
*Kwa kauli ya Nabiya.* (ubeti wa 594)

*La kwanza kuwa na dari,*
*Njema mno ya fakhari,*
*Ya kupendeza nadhari,*
*Mtu akiyangaliya.* (ubeti wa 595)

Kwa ujumla, urudiaji wa kisufi ni mtindo ambao umetumiwa kuendeleza dhamira ya toba, utakatifu, suala la dini, maangamio na hukumu katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimu*. Mtindo huu wa urudiaji wa kisufi umemwezesha mtunzi kuendeleza mawazo yake kuhusu dini, kuleta maana, kudhihirisha hisia na

hali mbalimbali katika utenzi huu na kwa jinsi hii kukuza na kuendeleza fani na maudhui ya utenzi huu.

Isitoshe, katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* mambo haya yanayohusu usufi yamezungumziwa kwa kurudiwarudiwa. Mambo haya yamezungumziwa kwa kurudiwa mtunzi anapotuelezea kuhusu majukumu mbalimbali katika Uislamu. Usimulizi huu ni muhimu kwa sababu unasaidia katika kuimarisha imani ya msufi katika dini.
Katika utenzi huo, msimulizi anaeleza kuwa kuna vitu vinne tu ambavyo vikizingatiwa na msufi basi atapata fursa ya kwenda peponi bila kupingwa. Mambo haya manne yakifuatwa na msufi bila shaka hata Mungu hufurahia alipo. Mosi, msufi anapaswa kuwa na subira. Hili litamwezesha mtu kuvumilia shida na hasara. Pili, msimulizi anaendeleza usimulizi huu kwa kueleza ya kwamba msufi anastahili kuwa na akili imara. Akili nzuri ni muhimu sana kwa vile itamwezesha msufi kutafakari. Msufi akiwa na uwezo wa kufikiri basi atajiepusha na maovu kwa vile ataweza kutofautisha kati ya mambo mazuri na mabaya. Tatu, msufi anastahili kuwa mwenye kuona haya kila wakati. Msufi mwenye haya atafahamu mambo ya kunena mbele ya watu. Kwa hivyo, hatajivua nguo au hata kuwavua wenzake nguo.

Msufi huyu atajiepusha na aibu mbele ya watu. Isitoshe, watu hawataaibika wakiwa naye. Jambo la nne linalodokezwa na msimulizi ni kuwa msufi anastahili kuwa mtu mwenye elimu. Kwa sababu ya elimu, atafahamu mambo mbalimbali duniani. Hili litazuia kuhadaiwa kwake na watu wabaya. Vilevile, msufi ana maarifa yanayohusu mambo mbalimbali kwa mapana. Mambo haya yote manne yakizingatiwa na msufi, basi Mungu na Mtume watamfurahia. Usimulizi wa masuala haya umeibua dhamira ya adili, elimu, subira, haya, ukarimu na toba. Maudhui haya yamerudiwarudiwa katika utungo huu na kwa njia hii kujenga usufi na kuendeleza urudiaji. Mambo haya yanasimuliwa katika beti hizi:

*Mambo mane Isilamu,*
*Awapo nayo ni tamu,*
*Tena imetulazimu,*
*Kwa kauli ya Nabiya.* (ubeti wa 594)

*La kwanza kuwa na dari,*
*Njema mno ya fakhari,*
*Ya kupendeza nadhari,*
*Mtu akiyangaliya.* (ubeti wa 595)

*La pili firasha ali,*
*Tukufu zenye jamali,*
*Zisokuwa na mithali,*
*Hapa katika duniya.* (ubeti wa 596)

*La tatu nguwo taibu,*
*Kuwa nazo ni wajibu,*
*Ukavaa kwa ajabu,*
*Haiba ikaeneya.* (ubeti wa 597)

*Na la nne tawakhubiri,*
*Ni taa ya kunawiri,*
*Nuru zenee dahari,*
*Uwashapo yako taa.* (ubeti wa 598)

**7.0 Motifu Kama Mtindo katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi***

Katika uchunguzi wa motifu katika utenzi huu, tumeongozwa na Nadharia ya Umitindo. Nadharia hii imetusaidia katika kubainisha namna mwandishi alivyokiusha lugha yake kwa kutumia muundo wa ishara uliorudiwa kuwasilisha dhamira na maana kwenye utungo. Abbott (2008) anafafanua kuwa motifu ni taswira ama kifungu cha maneno yanayorudiwa katika masimulizi. Naye Elizabeth (2021) anaeleza motifu kama muundo unaorudiwa kama picha, sauti, neno au ishara katika kazi ya kifasihi ili kusisitiza dhamira. Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, motifu mbalimbali zimewasilishwa kupitia urudiaji wa muundo wa ishara.

Nurbakhsh (1986) anafafanua kuwa ishara kama vile safari, mwanga na ndege ni udhihirisho wa siri za Kimungu katika kiwango cha ufahamu kupitia ibada ya nafsi pamoja na fikra za akili. Kwa hivyo, ishara inawakilisha maana ya ndani ya matamshi ya nje ambayo huleta utambuzi wakati unapoambatishwa na mambo ya Mungu. Asili ya ukweli wa ishara inajumuisha ukweli wa kighaibu ambao unaletwa na utofauti mdogo wa ujuzi ulioelezwa kwa siri kupitia ulimi wenye ufahamu wa ndani.

Nurbakhsh (1986) anasema kuwa masufi wamebuni tamathali za usemi mbalimbali ili kuashiria vitu na sifa za watakatifu au wapendwa katika ushairi. Kila ishara ina tafsiri yake maalumu inayowakilisha sifa za yule wa kipekee kama vile Mtume Muhammad, Mungu na mafumbo ya safari ya kiroho yanayomhusu msafiri wabinafsi kwa Mungu. Kulingana na masufi, Mungu alimuumba Adamu kwa mfano wake. Kauli hii imekuwa ikitumika kama ishara ya sitiari inayowapa mamlaka ya kimaandishi watunzi wa ushairi. Kuna sababu tatu za msingi zinazoelezea ni kwa nini washairi wa sufi walichukua hatua hii:

Kwanza, washairi wa kawaida walitumia picha za wapendwa na vitu mbalimbali kama vile nambari, ndege, safari na kadhalika kama ishara inayoonesha kuwa wana lugha inayotumia maneno ya kifahari wanapojieleza. Ishara hizi zilikuwa na ufanisi katika kukuza mvuto katika mashairi ya kimapenzi. Kwa kutumia taswira za aina hii, masufi waliweza kutoa maelezo yao ya kishairi kuhusu kuwa katika

umoja na Mungu kwa njia dhahiri au wazi huku wakionesha uzuri wake kupitia matumizi ya ishara kama vile ishara ya ndege kama ilivyo katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Hili liliwawezesha kutumia vipengele vinavyounda taswira inayoeleza kitu kinachopendeza au kinachopendwa cha jitihada za msafiri.

Pili, taswira na mafumbo kama haya hupenya na kuchochewa moyoni kwa urahisi zaidi kuliko maneno ya kifalsafa ya kifikra. Masufi wanaamini kuwa matumizi ya taswira na mafumbo yanawasaidia katika kumudu ufahamu wao wa kina na wa haraka zaidi kuhusu sifa na uwezo wa Mungu. Kwa kutumia sitiari na mafumbo, masufi wameweza kueleza hali yao ya kiroho kwa watu wengine.

Tatu, mafumbo haya yamewafaidisha masufi kwa kuwawezesha kulinda siri zao za safari ya ndani ili isijulikane kwa watu wasio masufi. Aidha, kupitia mafumbo haya, masufi wamehakikisha kwamba wenye ujuzi na uzoefu halisi wa hali ya kiroho katika usufi ndio wanaelewa kikamilifu kile kinachoelezwa kwa kutumia ishara.

Sufi wamechukua maneno yanayotumiwa kuelezea ishara, hali na kuonesha upendo kwa kutumia tamathali mbalimbali kwa madhumuni ya kuwasilisha asili ya upendo wa ukweli. Tamathali hizi ambazo polepole zilianza kuingia katika ushairi wa kisufi na nathari hazikutumiwa tu kuwasilisha ujumbe wa usufi kwa uzuri. Pia, zilitumiwa kueleza fikra zao kwa upendo wa kiroho kwa njia rahisi na ya kuvutia. Katika utenzi huu, sawa na tungo tofautitofauti za Kiswahili, dhana ya usufi imefungamanishwa na ishara mbalimbali. Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* motifu hizi ni pamoja na: safari, ndege na mwanga. Utafiti huu umeshughulikia motifu hizi kama mtindo wa urudiaji unaotumiwa na mtunzi kuwasilisha dhamira mbalimbali. Aidha, mtindo huu unaohusisha matumizi ya motifu ndio msingi wa maana inayowasilishwa na mtunzi.

### 7.1 Motifu ya Safari

Masufi mbalimbali wanakubaliana kwamba lengo la usufi ni katika safari, lakini njia wanazotumia kuafikia safari ni za kujadiliwa. Tunajadili aina mbalimbali za motifu ya safari ambazo zimesheheni katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Katika kufanya hivyo, tumeongozwa na Nadharia ya Umitindo. Nadharia hii inatusaidia katika kuchunguza kisemwacho na namna kinavyosemwa. Wazo hili limetusaidia katika kuchunguza namna mtunzi anavyotumia motifu kama njia ya kufanikisha fani na maudhui katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Motifu hizi ni pamoja na:

#### 7.1.1 Motifu ya Safari ya Ndani

Wa Mutiso (2005) anafafanua kuwa katika usufi, dhana ya safari ya ndani hurejelea ile hali ya kujitambua na kumkaribia Mwenyezi Mungu. Katika safari

hii, mambo mbalimbali anayokumbana nayo msufi yanaongozwa na kudhibitiwa na Mungu. Ili msufi aweze kufikia safari ya ndani, ni lazima atubu dhambi zake na kumrejelea Mungu. Safari hii ya ndani hufikiwa kutokana na kujitenga na dhambi kwa vyovyote vile na kuishi maisha yanayoongozwa na Mungu. Maisha haya humlazimisha msufi kujitenga na mambo yote ya kidunia. Aidha, msufi huafikia safari ya ndani anapokuwa na subira wakati wa majaribu na kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu wakati wa mafanikio. Safari ya ndani vilevile huendelezwa wakati msufi anapoyaonesha mapenzi yake kwa Mungu kupitia mashairi na nyimbo.
Mtunzi wa utungo huu anaeleza kwa kurudia kuwa ili Mwislamu aweze kufikia safari ya ndani, ni lazima akubali kubadili maamuzi yake ya kiroho. Kufikia hali ya kubadili maamuzi ya kudumu ndiyo lengo kuu la usufi. Kauli hii inachangia dhamira ya dini *katika Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*. Usimulizi huu unachangia katika kumshinikiza Mwislamu kutubu na kufuata sheria za Mwenyezi Mungu. Msufi lazima abadili uamuzi wake wa wito katika utawa ili amkumbuke Mungu. Kwa mfano, katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, Mwislamu ametengewa siku na miezi ya kufunga na kuomba kama njia ya kumrudia Muumba wake.

Katika kipindi hiki, Mwislamu hastahili kuvunja kufunga kwake. Aidha, anastahili kuomba kila wakati kama njia ya kumrudia Muumba wake na hata kumshirikisha Mungu kwa kila jambo analolifanya. Usimulizi huu umejadiliwa kwa kurudiwarudiwa katika utungo huu. Isitoshe, ni usimulizi ambao umesheheni katika tungo nyinginezo za kidini kama vile *Utenzi wa Qiyama* na hata *Utenzi wa Ayubu* na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza usufi.

Katika ubeti wa 4-53, mtunzi anaeleza kuwa Mungu aliumba miezi minne mitakatifu. Mwezi wa Muharamu, Rajabu, Shaabani na Ramadhani. Mtunzi anasimulia kuwa Mwislamu anastahili kufunga na kuomba wakati wa miezi hii mitakatifu. Vilevile, Mungu aliumba siku nne takatifu. Siku ya Juma, Idi mbili na Arafa. Mtunzi anasisitiza kuwa baada ya siku hizi nne takatifu kuumbwa, Mungu aliwatengea Waislamu siku bora. Siku hizi zinastahili kuheshimiwa, na Waislamu wote wanapaswa kutii vilivyo kwa kuomba katika siku hizo ambazo ni Lailatu I'Haji, idi na Laila Miiraji. Mifano katika utenzi;

*Nyezi nne fahamuni,*
*Alizoumba Mannani,*
*Kateuwa Rahhamani,*
*Mine kayakhitariya.* (ubeti 48)

*Na masikuiliyo bora,*
*Aliyotenga Jabara,*
*Taweleza kula mara,*
*Mtakapo kusikiya.* (ubeti 52)

Isitoshe, katika utungo huu, Mwislamu anaonekana kusoma na kufahamu sheria za kufuata kwa mujibu wa dini. Sheria hizi ni pamoja na kujisalimisha kwa Mungu, uaminifu, kujitolea, umakini, heshima na kuegemea upande wa Mungu. Vilevile, mtunzi anaelezea kuwa Mwislamu ana uwezo wa kufikia safari ya ndani kutokana na tabia zake ambapo Mwislamu anashauriwa kuwa na nidhamu, ubinafsi na sifa zinazostahili.

Zaidi ya hayo, mtunzi wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* amemshauri Mwislamu kuwa ni vyema awe na utakatifu. Mwislamu anasisitiziwa kuwa ili aweze kuafikia kiwango hiki ni lazima awe na nguvu za kiroho zinazoonekana wakati roho ya mtu inapoinuliwa. Mtunzi vilevile anasema kuwa kuna mtazamo wa siri, usafi, furaha, siri, uhamisho na utulivu katika kiwango hiki. Aidha, Mwislamu ameshauriwa na mtunzi kusahau nafsi yake ya kimwili na kumfuata Mungu hata kimatendo. Mtunzi anasisitiza kuwa katika hali hii halisi, Mwislamu huanza kwa kufunua, kutafakari, kutazama, kupanua, kuungama na kutangamana.

Katika utungo huu, mtunzi anaelezea kuwa Mwislamu anatarajiwa kuwa na lengo kuu ambapo anatarajiwa kuwa na umoja na Mungu. Mwislamu anahimizwa kuangazia ubinafsi wake, utambuzi, uficho, ugunduzi, upweke, mkusanyiko na umoja. Safari hii ya ndani imeangaziwa katika matukio na vitushi mbalimbali kama vile kisa cha Abubakari, hadithi ya Ibilisi, kisa kinachohusu kifo cha Mtume Muhammad, hadithi ya mambo manne muhimu kwa Mwislamu, hadithi ya Nuhu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza usufi katika utungo huu.

### 7.1.2 Motifu ya Safari ya Nje

Geoffrey (2010) anaeleza kuwa safari ya nje katika usufi hurejelea safari ya kidunia inayohusu mambo yale anayokumbana nayo msufi ama anayokutana nayo katika maisha. Mtunzi wa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* ameangazia suala la safari ya nje katika kazi yake kwa njia sawa na tungo nyinginezo za kidini. Motifu ya safari ya nje imeangaziwa katika vihadithi mbalimbali kama vile hadithi ya Mtume Muhammad, hadithi ya Habila na Kabila, hadithi ya Ali bin Abi Talibi, hadithi kuhusu majukumu mbalimbali katika Uislamu, hadithi ya Firauni na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza usufi katika utungo huu. Safari hii inatokea wakati mtunzi anapozungumzia vifo vya watu mbalimbali kwenye utungo.

Kwa mfano, katika ubeti wa 235-258, mtunzi anaelezea namna ambavyo mhusika Kabila alimuua nduguye Habila baada ya Habila kukataa asimuoe. Baada ya kifo cha Habila, nduguye alimzika kando ya mto na kaburi lake kufunikwa kwa maji. Kisa hiki ni mfano wa safari ya nje kwenye utungo huu.

*Hao wana wa Rasula,*
*Taweleza kwa ajili,*
*Ni Habila na Kabila,*
*Habila kajifiliya.* (ubeti wa 240)

*Na Kabila maanaye,*
*Kani kuu ushishiye,*
*Taka kumuoa nduye,*
*Walotoka mimba moya.* (ubeti wa 242)

Vilevile, mtunzi ameangazia vifo vya jeshi la Firauni baada ya kuangamizwa na Nabii Musa kwa kukataa kufuata sheria za dini ya Kiislamu, (ubeti wa 298-332). Safari ya nje vilevile imeshughulikiwa na mtunzi anapowaelezea Waislamu kuwa ni lazima mtu afe katika kisa kinachohusu majukumu mbalimbali katika Uislamu (ubeti wa 592-665) na kisha baadaye roho yake ifufuke siku ya kiyama kwa ajili ya hukumu. Mifano hii inadhihirisha kuwa *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* sawa na tenzi mbalimbali za kidini zimetawaliwa na motifu ya safari. Urudiaji wa motifu ya safari katika vihadithi mbalimbali kama tulivyotaja hapo juu unachangia katika kujenga urudiaji na kukuza usufi katika utenzi huu.

### 7.1.3 Motifu ya Ndege

Nurbakhsh (1986) anaeleza kuwa ishara ya ndege katika tungo za dini ya Kiislamu ni muhimu. Ishara hii imejumuishwa katika ishara maarufu miongoni mwa ishara zingine kama vile divai, waridi na bustani. Ishara ya ndege imeangaziwa katika matukio na vitushi mbalimbali kama vile kisa cha Abubakari, hadithi ya Ibilisi, hadithi ya uumbaji, hadithi ya mambo manne muhimu kwa Mwislamu, hadithi ya Nuhu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza usufi.

Ishara ya ndege imetumiwa katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* mtunzi anapoelezea kuwa Mungu aliumba ndege na wanyama wengine wa kupaa angani baada ya kuumba vitu vinne vitakatifu. Katika utungo huu, sawa na tungo nyinginezo za kidini, ndege ametumiwa kwa maana mbalimbali kama vile ishara ya nafsi. Ndege pia ametumiwa kama ishara ya watu wengine, uzoefu na uumbaji. Katika utenzi huu, Mwislamu anayejitenga huashiria ndege katika ngome ya uhamisho huku Mwislamu aliyeuawa ameashiriwa na ndege mtakatifu aliyerejea kiotani. Mwislamu aliyeuawa ameashiriwa na ndege walio kimya huku mitume, malaika na watakatifu wakiashiriwa na ndege wanaopepea katika bustani ya mbinguni.

Kwa kweli picha ya ndege wanaoruka imetumiwa katika tungo hizi za kidini sawa na *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* kama ishara ya roho ya mwanadamu inayoinuka kuelekea juu. Ulinganishi wa roho ya mwanadamu na ndege ni dhana ya kawaida kwa Waislamu. Mfano katika utungo:

> ***Akaumba na tuyuri**,*
> *Wenye mbawa akhiari,*
> *Abiadhi ahadhari,*
> *Ahmari suwadiya.* (ubeti wa 62)

Katika ubeti huu, mtunzi anaelezea kuwa Mungu aliumba ndege wengi wenye mabawa na kuwaweka duniani. Matumizi ya ishara ya ndege katika ubeti huu, sawa na vihadithi mbalimbali kama tulivyoeleza hapo juu, yamechangia katika kujenga urudiaji na kwa jinsi hii kukuza usufi katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*.

### 7.1.4 Motifu ya Mwanga

Katika tungo za Kiislamu, Mwenyezi Mungu ndiye nuru ya msingi isiyo na kifani ya ulimwengu. Mwenyezi Mungu ndiye nuru safi ya mwanzo wa mbingu na ardhi. Mwenyezi Mungu ndiye nuru muhimu iliyowekwa ndani ya roho na mwili (Wa Mutiso, 2005). Mutiso anasisitiza kuwa kwa mujibu wa watunzi wa tungo za Kiislamu, Mwenyezi Mungu aliumba ulimwengu ambapo nuru inaweza kuonekana dhidi ya giza. Suala hili limeangaziwa katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* hasa mtunzi anapozungumzia hadithi ya uumbaji wa vitu mbalimbali katika ubeti wa 33-63. Katika beti hizi, mtunzi anasisitiza kuwa Mungu aliumba nuru iliyong'ara dhidi ya giza. Kwa mfano:

> *Akaumba na Kamari,*
> *Na shamzi anuwari,*
> *Na nyota ziso kadiri,*
> *Mushitara na dhuriya.* (ubeti wa 63)

Suala la mwanga na Mungu kupewa sifa ya kuwa nuru limeangaziwa kwa kiasi kikubwa katika tenzi za kidini kama vile *Utenzi wa Qiyama*, *Utenzi wa Ngamia na Paa* na hata katika *Utenzi wa Adamu na Hawa*. Katika dini ya Kiislamu, dhana ya nuru hurejelea mwangaza baridi wa usiku au mwanga usio na joto au mwanga wa mwezi (Nurbakhsh, 1986). Nuru hii inatumika katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* na tungo nyinginezo za kidini kama ishara ya mwongozo na ujuzi wa Mungu na ishara ya rehema. Katika utungo huu, Mungu ametajwa kuwa ni nuru ya mbingu na ardhi sawa na tungo nyinginezo za kidini. Mungu anaangazia ulimwengu kwa ufahamu.

Neno 'nuru' linatumika katika utungo huu kumrejelea Mungu, Mtume Muhammad, *Kuruani*, mwezi, wanaume na wanawake waaminifu ilhali neno 'giza' linatumika ili kumrejelea shetani na kafiri (asiye amini katika dini ya Kiislamu). Vilevile, neno 'giza' hurejelea harakati ya kutoka gizani kwenda kwenye nuru na kutoka katika ujinga kuingia kwenye imani. Neno 'nuru' pia

linatumika kurejelea maana mbalimbali kama vile dini ya Kiislamu, imani, amri za Mungu na sheria za maadili katika *Kuruani*, mwanga wa mchana, nuru ya mwongozo ambayo Mungu atawapa waaminifu siku ya urejesho, amri za *Kuruani*, haki na nuru ya mwezi. Kwa masufi, mwangaza ni uumbaji wa kwanza wa Mwenyezi Mungu na vitu vingine vyote na viumbe vilivyoumbwa baadaye vinatoka kwa nuru. Nuru ilikuwapo kabla ya uumbaji.

Isitoshe, Wa Mutiso (2005) anaeleza kuwa vitu vyote viliumbwa kutoka kwa nuru. Ulimwengu ni udhihirisho wa nuru iliyowekwa katika mwili wa Adamu na manabii kama vile Mtume Muhammad, Nabii Isa, Nabii Musa na kadhalika. Uumbaji ulianza na nuru Muhammad. Mungu alitoa nuru kutoka moyoni mwake. Asili ya nafsi ni nuru kamili, hakuna nyingine. Kauli hii inaleta maana ilikuwa nuru ya Muhammad.

Katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi*, Waislamu wanatumia neno nuru ili kuwakilisha kile tunachojua ndani yetu (Wa Mutiso, 2005). Kuna nuru inayofichua ukweli kamili, nuru ya akili na nuru ya maumbile. Uwepo wa Mwenyezi Mungu ndio asili ya nuru ya uumbaji. Uwepo wa nuru hii huangazia dunia daima. Nuru ya Mwenyezi Mungu huangaza ulimwengu wote kwa uzuri mwingi na ukamilifu. Ili kuangaziwa na nuru hii, ni lazima upate wokovu.

Mwanga wa kiroho hutiririka kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine kwa njia ya upendo. Kulingana na Waislamu katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* na tungo nyinginezo za kidini, nafsi inarejelea mwanga wa jua. Malaika ambao hawana miili wametoka katika nuru ya jua la roho ya Mungu. Hivyo basi, nafsi zote zimeumbwa kwa nuru. Motifu ya mwanga imeangaziwa katika matukio na vitushi mbalimbali kama vile kisa cha Abubakari, hadithi ya Ibilisi, kisa kinachohusu kifo cha Mtume Muhammad, hadithi ya Siku ya Qiyama, hadithi ya mambo manne muhimu kwa Mwislamu, hadithi ya Nuhu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza usufi. Kwa mfano;

*Ya Muinu aunaka,*
*Wahaduhu la sharika,*
*Ndiye mwenye mamlaka,*
*Ya akhera na duniya.* (ubeti wa 15)

*Tamsifu Mola wangu,*
*Ndiye Mukhuluku mbingu,*
*Kahuyi na ulimwengu,*
*Shaka na gharibiya*. (ubeti wa 16)

*Ndiye Muhui nafusi,*
*Ndiye wa kutunafusi,*
*Na Arishi na Kurusi,*

*Zote akatuwekea.* (ubeti wa 17)

*Ndiye Muhui lahamu,*
*Kaitiya na idhambi,*
*Mishipa yote na damu,*
*Zikakutana pamoja.* (ubeti wa 18)

*Mtume wetu ni taa,*
*Nuru imezozagaa,*
*Mezowekewa Shufaa,*
*Umati kushufaiya.* (ubeti wa 68)

*Mtume wetu ni Twaha,*
*Mtia muili swiha,*
*Wajihika msobaha,*
*Hupendeza kwangaliya.* (ubeti wa 70)

*Mtume wetu Habibu,*
*Ndiye nuru ya kalibu,*
*Sharikati na gharibu,*
*Alipowa ni hidaya.* (ubeti wa 72)

Katika mifano hii, mtunzi anasisitiza kuwa Mungu ndiye nuru halisi ya mbingu na ulimwengu. Nuru yake inaangaza na tena inatibu. Vilevile, katika ubeti wa 68-72 mtunzi anaeleza kuwa Mtume Muhammed ndiye taa inayomulika na hata kuwaokoa Waislamu. Sababu yake ni kwamba nuru hii imewekewa shufaa. Vilevile, mtunzi anasisitiza kuwa nuru ya Mtume Muhammad inamulika roho ya Waislamu na hata kuosha dhambi zao. Hivyo, motifu ya mwangaza imeangaziwa katika vihadithi mbalimbali kama tulivyotaja hapo juu na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kukuza usufi. Kwa ujumla, motifu ya safari, mwanga na ndege zimetumiwa kama mtindo wa urudiaji unaowasilisha dhamira mbalimbali kama vile uumbaji, hukumu na toba. Aidha, mtindo huu unaohusisha matumizi ya motifu ndio msingi wa maana inayowasilishwa na mtunzi kupitia ujenzi wa wahusika kama vile Mtume Muhammad, Mungu na Waislamu.

**8.0 Hitimisho**

Katika makala hii tumeshughulikia dhana ya urudiaji na usufi katika utenzi wa Kiswahili. Pamoja na hayo tumeshughulikia motifu mbalimbali zinazorudiwa kupitia matumizi ya muundo wa ishara. Tumebainisha kuwa matumizi ya urudiaji wa kisufi katika *Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi* yanachangia uwasilishaji wa maana na ukuaji wa fani na maudhui katika utungo huu. Kwa upande mwingine, mtunzi wa utenzi huu amedhihirisha matumizi ya motifu mbalimbali za usufi katika utenzi huu. Motifu hizi za usufi zimerudiwa katika vihadithi mbalimbali katika utenzi huu na, kwa jinsi hii, kujenga urudiaji na kukuza usufi. Sifa hizi zinachangia katika kukuza dhamira ya hukumu, toba, siku

ya kiyama na maudhui mbalimbali ya kidini katika utungo huu sawa na tungo nyinginezo za kidini na kwa jinsi hii kujenga urudiaji na kuendeleza usufi pamoja na umuhimu wake. Zaidi ya hayo, tumegundua kuwa mtindo unaohusu urudiaji wa kisufi, motifu pamoja na vipengele vyake ndio msingi na kiini cha fani na maudhui katika utungo huo.

**Marejeleo**

Abbott, H.P. (2008) *The Cambridge Introduction to Narrative*. Cambridge: Cambridge University Press.

Abrams, M.H. (2015) *A Glossary of Literary Terms*. New York: Cengage Learning, Inc.

Al-Bukhari, M. (1989) *Hadith of the Prophet*. Cairo: Al-Azhar Publisher.

Aloo, R. na Wa Mutiso. K. (2023) "Urudiaji wa Kisimulizi na wa Kisemantiki kama Mtindo katika Tenzi: Utenzi wa Seyidina Ali na Mudhari bin Darimi". *Jarida la Mwanga wa Lugha*, Juz. Na. 8(2): 17-24. Inapatikana katika https://journals.mu.ac.ke/index.php/mwl/article/view/333. Ilisomwa tarehe 12 Februari 2025.

Chapman, A. (1974) *Jewish – American Literature*: *An Anthology*: West Bengal: Signet Press**.**

Croft, S. na Robert, M. (2000) *Exploring Language of Literature*. London: Oxford University.

Crystal, D. na Davy, D. (1969) *Investigating English Style*. London: Longman Group.

Elizabeth, D. (2021) *Oregon State Guide to English Literary Terms*. Oregon: Oregon State University.

Geoffrey, E. (2010) *Introduction to Sufism*: *The Inner Path of Islam*. New York: World Wisdom, Inc.

Knappert, J. (1964) *Four Swahili Epics*. Leiden: E. J. Brill.

Leech, G.N. (1969) *A Linguistic Guide to English Poetry*. London: Longman Group.

Nurbakhsh, J. (1986) *Sufi Symbolism*. London: Khaniqahi-Nimatullah Publications.

Schaeder, H.H. (1935) *The Interpretation of Islamic Mysticism*. New York: Cambridge University Press.

Simpson, P. (2004) *Stylistics*. *A Resource Book for Students*. London: Routledge.

Tannen, D. (1989) *Talking Voices*: *Repetition*, *Dialogue and Imagery in Conversational Discourse*. New York: Cambridge University Press.

Wamitila, K.W. (1999) "A Rhetorical Study of Kiswahili Classical Poetry: An Investigation into the Nature and Role of Repetition". *Research in African Literatures*. Bloomington: Indian University Press. Tol. 30(1). kur. 58-73.

Inapatikana katika https://www.africabib.org. Ilisomwa_tarehe 15 Februari 2025.

Wamitila, K.W. (2003) *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K.W. (2008) *Kanzi ya Fasihi*: *Msingi wa Uchanganuzi wa Kiswahili wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Ltd.

Wa Mutiso, K. (2005) *Utenzi wa Hamziyya*. Dar es Salaam: TUKI.